JARIDA LA BENKI YA POSTA

Truly Tanzanian

Januari - Marchi 2009 | Jarida la ndani | Toleo la 1

Habari na Picha

BENKI YA POSTA YAPATA MWENYEKITI MPYA WA BODI.

Benki ya Posta imepata mwenyekiti mpya wa bodi ya Wakurugenzi. Mwenyekiti huyo ni Profesa. Leticia Rutashobya, (katikati walioketi) ambaye pia ni mhadhili katika chuo kikuu cha Dar es Salaam kitivo cha Biashara. Profesa Leticia anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Bw. Kapellega ambaye amemaliza kipindi cha miaka mitatu ya uongozi. Pia bodi imemkaribisha mjumbe mwingine mpya wa bodi, Bw. M.G Kamugisha ambaye anatokea kwenye wizara ya fedha na uchumi.

MABADILIKO YA MICHANGO YA WANACHAMA WA MFUKO WA KUFARIJIANA.

Mfuko wa Kufarijiana ni mfuko wa hiari wa wafanyakazi wa Benki ya Posta Tanzania ambapo michango hukusanywa kila mwezi kutoka katika mishahara ya wafanyakazi. Mfuko huu unaendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizokubaliwa na wanachama wote wa mfuko. Katika Mkutano wa Kufarijiana wa Wafanyakazi wa Benki ya Posta Tanzania uliofanyika tarehe 12.1.2009 katika ukumbi wa Mhasibu, Dar es salaam, pamoja na mengine, maamuzi yafuatayo yalifikiwa;

- Michango ya wanachama ya kila mwezi imeongezwa toka Sh. 3,000/= hadi Sh. 5,000/= Faraja zote kama zilivyoainishwa kwenye katiba ya mfuko wa kufarijiana zimeongezwa kama ifuatavyo;
- Faraja kwa kufariki mwanachama imeongezwa toka Sh.500,000/= hadi Sh.700,000/=
- Faraja ya mwanachama kufiwa na mtegemezi (Baba, Mama,Mume,Mke na Watoto) imeongezwa toka Sh.300,000/= hadi Sh.450,000/=
- Faraja ya kufiwa na ndugu katika kituo cha kazi imeongezwa toka Sh.100,000/= hadi sh.150,000/=
- Faraja maalumu ya matukio mengineyo imeongezwa toka Sh.50,00/= hadi Sh.100,000/= Kiingilio kwa mwanachama yaani mfanyakazi anayeajiriwa imeongezwa toka Sh.10,000/= hadi Sh.20,000/. Pia atatakiwa kukatwa Sh.5,000/= kama mchango wake wa kawaida wa mwezi. Mabadiliko haya yameanza kutekelezwa tarehe 1.2.2009.

BARAZA

Mkurugenzi mtendaji wa Benki ya Posta Alphonse Kihwele (katikati waliokaa)katika picha ya pamoja na wajumbe wengine wa Baraza la wafanyakazi wa Benki ya Posta.

Baraza la wafanyakazi wa Benki ya Posta lilikutana tarehe 12/12/2008 ili kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili wafanyakazi wa Benki hiyo. Mkutano huwo wa mwaka chini ya Afisa mtendaji mkuu wa Benki ya Posta Alphonse Kihwele, pamoja na mambo mengine pia uliwakaribisha wawakilishi wapya wa baraza waliochaguliwa baada ya kuisha kipindi cha miaka 3 ambacho wawakilishi wa baraza la zamani walitumikia.

MAHAFALI Rugambwa Sec School.

Meneja wa Benki ya Posta tawi la Bukoba Bw. Maduhu Makoye, aliombwa na uongozi wa Rugambwa Secondary School kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya kidato cha Nne, yaliyofanyika tarehe 30/01/09. Wakati wa mahafali hayo, Bw.Makoye alitoa zawadi mbali mbali kwa wahitimu na pia kwa shule hiyo kwa ujumla. Zawadi zilizotolewa ni pamoja na mipira 3 kwa ajili ya michezo ya pete, kikapu pamoja na mpira wa wavu. Wanafunzi watatu waliofanya vizuri kwenye masomo yao walipata zawadi maalum kutoka benki ya posta,ambayo ni kufunguliwa akaunti na kuwekewa kiasi cha sh. 20,000/= kwenye akaunti ya kila mmoja wao.Shule hii ina uhusiano wa karibu na wa muda mrefu na Benki ya Posta, kwani wanafunzi na walimu wa shule hii ni wateja wazuri wa Benki ya Posta. Wengi wao wamefungua akaunti na pia wamepata mikopo kutoka Benki ya Posta.

TUJIKUMBUSHE MALENGO YETU

Dira Yetu (Vision)

"Kuwa Benki teule ya Wananchi."

Azma Yetu (Mission Statement)

"Ni kutoa huduma za kibenki kwa watu wenye kipato cha chini, wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati, wakati huo huo kujenga thamani kwa wadau."

GAZEBO CAMPAIGN MBEYA

Wafanyakazi kutoka tawi la Mbeya wakiwa kwenye Gazebo tayari kwa kuhudumia wateja.

WESTERN UNION YAZINDUA KAMPENI IITWAYO "GO EAST AFRICA"

Meneja Mwandamizi wa huduma za Western Union Bw.Kolimba Tawa Akizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni ya "Go East Africa".

Tarehe 24th Desemba 2008, Western Union ikishirikiana na Tanzania Postal Bank pamoja na maajenti wengine, walizindua promosheni iitwayo GO EAST AFRICAN. Katika promosheni hii,mteja yeyote atakaetuma au kupokea pesa kutoka nchi za Uganda, Kenya, DRC, na Rwanda na pia ndani ya Tanzania kwa kupitia mtandao huu wa Western Union anapata nafasi ya kujishindia kiasi cha Tshs.1 million kwenye droo ndogo au kiasi cha shilingi milioni4 kwenye droo kubwa itakayochezeshwa hapo baadae. Mbali na zawadi hizo, pia kuna zawadi nyingine nyingi za kushindaniwa kama vile simu za mkononi na zawadi za papo kwa papo pindi mteja atakapotumia huduma yoyote ya Western Union Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni, promosheni hii iliishirikisha Benki ya Posta pamoja na maajenti wengine, kama vile BOA bank, Kenya commercial bank (KCB) pamoja na Diamond Trust Bank. Kwa upande wa Benki ya Posta wateja walijishindia pesa taslim kama ifuatavyo kwenye droo kubwa iliyofanyika tarehe 13 March.

- Washindi watatu (3) walijishindia shs.4,000,000/= kila mmoja.
- Washindi thelathini (30) walijishindia simu aina ya Nokia 1200

Utoaji wa zawadi hizi kwa washindi waliojishindia pesa taslimu utafanyika tarehe 17 Aprili 2009 kwenye hoteli ya Palm Beach jijini Dar es Salaam.

MAHAFALI TUMEKUJA SEKONDARI ZANZIBAR

Meneja wa tawi la Benki ya Posta Zanzibar Bw.Bakari Kisuda alialikwa kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya shule ya sekondari ya Tumekuja. Hapa anaonekana akifurahia pamoja na mwalimu Mkuu wa shule hiyo Bi. Mgeni Mohamed Said, baada ya kukabidhi kiasi cha shilingi laki 5 kama mchango wa Benki ya Posta kwa shule hiyo ili iweze kununua mashine ya kudurufu.Mahafali hayo yalifanyika tarehe 7 Machi, 2009.

IJUE TUICO.

Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) ni chama kilichoundwa kwa tamko la Raisi wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania la mwaka 1970.

Katika mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi katika nchi yetu, yamesababisha kuwepo kwa haja ya kuwa na sheria mpya za kazi ambazo zitasimamia uhusiano sehemu za kazi katika mazingira mapya, katika sheria na. 6 & 7 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2004. Vyama vya wafanyakazi sehemu za kazi ndivyo vyenye nafasi ya:

1. Kujadili uboreshaji na kuendeleza hali bora za wafanyakazi katika maisha yao wakiwa kazini.
2. Kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kuunda kamati za majadiliano na kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi ili kudumisha amani mahali pa kazi.
3. Kujadili na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya mwajiri na mfanyakazi au mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya amani kila itakapowezekana.
4. Kujadiliana, kufunga, kusiamamia na utekelezaji wa mikataba ya Hali bora za kazi, Tuzo, kanuni za utumishi na sheria za kazi zitumikazo nchini.

MTOTO WETU HALIMA LIKUTU.

Mwezi Februari mwaka huu (2009), benki ilichukua jukumu la kumsaidia msichana Halima Likutu msaada wa kumlipia gharama za masomo na kumchukua kama sehemu ya familia ya TPB kutokana na aina ya matatizo aliyoyapata.

Kama sehemu ya msaada wa benki, pia amefunguliwa akaunti TPB ili kutoa nafasi kwa watu wengine wenye nia ya kumsaidia wasaidie. Akaunti hiyo ni:

Jina - HALIMA LIKUTU
Benki - BENKI YA POSTA TANZANIA
Tawi - TAWI LA MKWEPU
A/C No. 010-00224539

Wito: Endapo wasamaria wema watajitokeza kumsaidia tafadhali hizo ndizo taarifa za akaunti yake.

Pichani chini anaonekana Halima Likutu akipewa mkono na Mkurugenzi wa Radio One Deogratius Rweyunga, kwenye mkutano wa waandishi wa habari wakati wa kumkabidhi binti huyo mahitaji yake ya shule yaliyotolewa na Benki ya Posta. Radio One kupitia kipindi chao cha "Watoto waishio katika mazingira magumu" ndio waliotambulisha matatizo ya Halima kwa jamii, kilio ambacho Benki ya Posta ilikisikia na kuamua kusaidia

UHUSIANO WA CHAMA CHA WAFANYAKAZI NA UONGOZI WA BENKI YA POSTA TANZANIA.

Uongozi wa tawi la chama cha wafanyakazi Benki ya Posta Tanzania umekuwa na mahusiano mazuri na uongozi wa Benki. Uhusiano huu umewezesha viongozi wa tawi la chama kuwapatia wafanyakazi wengi elimu ya kuelewa umuhimu wa chama mahala pa kazi, lengo kuu likiwa ni kwamba, kwa kupiti chama cha wafanyakazi sehemu za kazi tumeweza kuunda mkataba wa Hiari pamoja na kujadili maslahi ya wafanyakazi kwa ujumla.

Matarajio ya uongozi wa tawi ni kwamba ushirikianouliopo kati yake na uongozi wa shirika hauna budi kuimarishwa zaidi ili kufikia lengo la mipango mbalimbali ambayo uongozi wa shirika umepanga kutekeleza kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa shirika na hatimaye kuinua kipato cha wafanyakazi wa Benki ya Posta Tanzania.

WITO WA UONGOZI WA CHAMA KWA WAFANYAKAZI WOTE WA BENKI YA POSTA TANZANIA.

Ndugu wafanyakazi, kipindi hiki cha mabadiliko makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu ya Tanzania, mabadiliko haya pia yamesababisha kuleta sheria mpya za kazi, sheria na. 6 & 7 ya mwaka 2004. Wafanyakazi ni muhimu muelewe kuwa bila kupitia uwakilishi wa chama kwa ajili ya majadiliano na mwajiri kwa namna yoyote ile itakuwa ngumu, hivyo uongozi unaomba wafanyakazi mjiunge na chama ili kuipata haki hiyo. Mfanyakazi popote alipo ni muhimu afanye kazi kwa kujituma ili kutimiza malengo, na kwa ushirikiano huo tutadai maslahi yaliyo bora zaidi.

TANGANYIKA YETU-MWAKA 1961

Baraza la kwanza la mawaziri la mwaka 1961 liliundwa na Mawaziri 12.Katika jarida letu hili nitakuwa nakuletea habari fupi za Mawaziri wa Baraza hilo la kwanza la nchi yetu,ili uweze kuwakumbuka na kuuenzi mchango mkubwa walioutoa katika kuijenga nchi yetu hata kufikia hapa tulipo.Mawaziri watatu(3) wataelezewa kwenye kila toleo.

Waziri Mkuu

BWANA JULIUS KAMBARAGE NYERERE,
Akiwa na umri wa miaka 39,na mwana wa Chifu, ndiye Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika. Baada ya kuelimishwa hapa Tanganyika,alikwenda Makerere College,Uganda,ambako alijipatia Shahada ya Ualimu,na katika Chuo Kikuu cha Edinburg ambako alijipatia Digrii ya "Master of Arts". Ni Rais wa TANU naye aliwakilisha mbele ya Umoja wa Mataifa mara mbili.

Waziri wa Fedha

SIR ERNEST VASEKY, K.B.E, C.M.G.
Akiwa mwenye umri wa miaka 60, alikuja Afrika Mashariki mwaka 1936;mara mbili aliwahi kuwa Meya wa Nairobi; na kutoka mwaka 1950 hadi 1959 alikuwa Mjumbe wa Lejiko ya Kenya. Aliteuliwa Waziri wa Fedha,Tanganyika, mwezi Februari,1960.

Waziri wa Mambo ya Sheria

CHIFU ABDULLAH SAIDI FUNDIKIRA,
akiwa mwenye umri wa miaka 40, alihitimu na kupata Shahada ya Kilimo huko Makerere College, Uganda,mwaka 1944.Mwaka 1953 alihudhuria mafunzo ya Kilimo katika Chuo Kikuu cha Cambridge. Aliteuliwa Waziri wa Ardhi na Upimaji mwezi Julai, 1959,na akawa Waziri wa Sheria mwezi Mei, 1961.

BENKI YA POSTA YASAIDIA UJENZI WA MADARASA.

Benki ya Posta siku zote imekuwa mstari wa mbele katika kutoa misaada mbalimbali kwa jamii, ili kuboresha hali ya maisha ya Mtanzania. Misaada hiyo imekuwa ikitolewa zaidi ili kuongeza nguvu na kasi ya kukua kwa uchumi, afya, kilimo na elimu, pamoja na masuala mengine mengi yanayoigusa jamii kwa ujumla.

Ndo maana Benki haikusita kutoa msaada wa kiasi cha shilingi milioni 5 kwa mbunge wa Kyela Mh. Harrison Mwakyembe,ili kusaidi ujenzi wa vyumba vya madarasa vya shule za sekondari za wilaya hiyo,ambayo mwaka huu wanafunzi takriban elfu 5 walifauli.Pichani,Mbunge wa Kyela Mh. Harrison Mwakyembe anaonekana akifurahia kupokea mfano wa hundi ya kiasi cha milioni 5 aliyokuwa akikabidhiwa na Meneja Uhusiano wa Benki ya Posta Noves Moses. Wa pili kushoto ni mwenyekiti wa Kyela Development Fund Gray Mwakalukwa,na pembeni yake ni meneja masoko wa TPB Andrew Chimazi.